**1013/1**
**P1 KISWAHILI**
**Karatasi 1**
**P.T.E.**
**March, 2019**
**Muda: Saa 2**

## MAAGIZO

Mtihani huu una sehemu: ***Insha, Ufahamu, matumizi ya lugha*** na ***sajili za lugha***
Ni muhimu sana ufuate maagizo uliyopewa mwanzoni mwa kila sehemu
Andika majibu yako kwenye nafasi ulizoachiwa
Usitoe karatasi yoyote katika kijitabu hiki.

**Kwa matumizi ya mtahini**

| Sehemu | Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|---|
| 1 | 1 | 20 | |
| 2 | 2 | 20 | |
| 3 | 3 | 30 | |
| 4 | 4 | 20 | |
| | 5 | 10 | |
| | | Jumla | |

**SEHEMU YA KWANZA: INSHA (ALAMA 20)**

1. Andika Insha isiyopungua maneno **350** kuhusu mojawapo ya mada zifuatazo:
   (a) Andika insha inayoanza kwa:
   Meli ilitia nanga hapo bandari ya Kilindini na manusura wa mkasa uliowasibu wenzao…………
   (b) Wajibu wa Tume ya Kusimamia Uchaguzi Mkuu Nchini Kenya kuhakikisha haki inatekelezwa.
   (c) Andika mazungumzo kati ya mwajiri na kitwana katika mazingira ya nyumbani.
   (d) Nangananga ya kuyu ndani kuna mabuu.

**2. SEHEMU YA PILI: UFAHAMU (Alama 20)**
**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali**

**MSALA**

Unadhifu wa msala ni jambo muhimu sana kwa sababu huwezesha afya nzuri kudumishwa kwa jumla na kwa mtu bi nafsi.

Kunayo misala ya umma ambayo imejengwa mijini ambapo wateja waliobanwa na haja huweza kutafuta huduma kutoka huko. Angaa siku hizi baadhi ya watu wabunifu wamekuja na wazo hili ambalo limenyosha mambo kidogo. Hapo awali raia walikuwa wakiteseka sana kwa vile wengine wangeonekana wamejibanza kutani **wakiziosha** na wasiojiweza kwa hili wangemalizia popote pale kwenye maeneo ya pembepembe na kufanya kila upitiapo kuwa fe! fe! fe!

Hali hii inadhihirisha kuwa kila mhitaji wa huduma hizi lazima awe na uwezo wa kiuchumi ambapo atachangia angaa shilingi tano, kumi au hata ishirini na zaidi ili kujiondolea **mbano** hasa mjini. Ulimwengu umekuwa nifae nikufae na hii kazi ya kutunza misala awali ingepewa kisogo lakini leo imekuwa chumo la juani ambalo huliwa kivulini. Bila shaka msala huhitaji kuhifadhishwa kwa kutumia maji, sabuni, brashi na vyombo vingenevyo ili mahali hapa pawe salama kutembelewa. Iwapo sehemu hii haitatunzwa nina uhakika harufu pekee haitamwezesha mtunzaji na wateja kupatembelea mahali penyewe kutafuta huduma. Isitoshe, tisho lingine kwa mhudumu wa mahali hapa ni maradhi yanayoweza kuathiri kila mhusika anayefika mahali hapa.

Ubaya wa baadhi ya wateja hudhihirika kutokana na matumizi mabaya ya misala kwa sababu ya ubinafsi wao na hali yao ya kutojali wenzao. Wengine huenda haja pasi kuondosha ile **mali** yao kwa kuyapiga maji. Nafikiri wengine hufanya hivyo maksudi ilhali wengine huwa ni kwa sababu ya kukosa uzingatifu au kwa sababu ya wao kuwa na pupa ya kuondoka wakitaka kwenda kushughulikia mambo mengine wakajikuta wameondoka huku wameacha mabaki yao. Ni vizuri kuangalia kwa makini mali uliyoiacha kuhakikisha imehifadhiwa mahali pake pasipo kuharibu msala.

Matumizi ya maji katika kujinadhifisha ni jambo linaloweza kufaa zaidi ili kuepuka kuambukizana maradhi kwa mtu binafsi. Inasikitisha kuwa utapata baadhi ya kuta za vyoo zimepakwa masizi kana kwamba wateja hawa hawakupewa shashi kimbele na mhudumu wa sehemu husika. Baadhi ya watu kama hawa wakitoka pembeni utawapata wako tayari kukupa salamu za mkono pasipo haya. Unawaji wa mikono unastahili kupewa kipau umbele baada ya haja kuhakikisha usafi unadumishwa.

Si wapakaji kuta pekee ambao huudhi bali hata wanaotumia vifaa vinginevyo mbali na zile shashi. Kunao wanaotumia vitambaa wakavibwaga kwenye kile kibakuli au kisahani cha msala na kusababisha kuziba kwa eneo hili. Wengine hutumia magazeti na kuchangia matatizo zaidi kwa wahudumu wa misala. Kunayo mambo mengi yanayoudhi kuhusu utumiaji wa sehemu hizi za pembeni yakiwemo kukawia mahali pale wakati wateja wengine wanahitaji **<u>kujifungua</u>**. Utamkuta mtu amejifungia mle ndani kwa dakika ishirini hadi thelathini na hata zaidi ambapo yule aliyemsubiri hapo nje hujiuliza iwapo mteja huyu anasoma kurasa za magazeti au anafanya nini!

Vilevile jambo la kutokalia lile bakuli la msala ni miongoni mwa matatizo ya utumiaji mbaya wa misala. Wateja fulani huamua kusimama kwenye mabakuli haya kwa sababu ya kutoamini kuyakalia. Hali hii inabainika wakati mteja mwingine anafika kutafuta huduma na kupata furushi la matope kwenye bakuli analotarajia kulikalia ambapo naye pia hulazimika kufuata mkondo kwa vile wahenga walisema **maji hufuata mkondo**. Kutokana na tukio hili ndio inakuwa rahisi kutumia mabakuli ya chini ya Kiasia kuliko yaliyoinuka ya Kiulaya.

Ingawa hivyo, mapinduzi ambayo yametokea katika sekta hii yameleta mabadiliko chanya ambapo matatizo yaliyokuwapo yamepunguka. Miaka ya awali ungewapata vijana wa mitaa wamemiliki sehemu hizi. Hawakujua kuzishughulikia sehemu hizi na hata wengine walikuwa wamefanya haya kuwa makao yao ambapo baadhi ya watu walioweza kuingia hapa wakitafuta kujisaidia walijikuta wameporwa bila habari. Wengine walitishwa kwa visu na kulazimishwa **kudondoka** mapesa ili kujisalimisha. Wale waliokataa kusalimu amri wakati mwingine walitishwa kupakwa masizi kutokana na mabaki hayo yaliyobebewa kwenye karatasi za plastiki au mikebe! Hali hii ni ya kuudhi zaidi na mara nyingi hutokana na uongozi mbaya wa serikali

za miji ambazo zikisimama kidete mambo kama haya hayawezi kutokea na raia wataweza kufurahia.
Usafi wa sekta hii ni muhimu na huletea miji yetu sura nzuri kwa wageni na wenyeji ndio sababu serikali za kaunti kwa ushirikiano na wizara husika ikiwemo ya afya, huduma za jamii, na nyinginezo ni muhimu kutekelezwa.

**Maswali**

(a) (i) Orodhesha tabia ZOZOTE TANO hasi za watumizi wa misala kwa mujibu wa kifungu hiki. (alama 5)

(ii) Kwa mujibu wa taarifa hii mwandishi anapendekeza suluhu gani kwa tabia hasi ulizodondoa hapa juu? (alama 5)

(b) Ni vifaa vipi vilivyotajwa kwa matumizi ya msalani kwa mujibu wa kifungu hiki? (alama 2)

(c) Watu wataathirika vipi kwa mujibu wa kifungu hiki iwapo msala utakosa kutunzwa vyema. (alama 2)

(d) Awali vijana wa mitaani walikera watumizi wa msala kivipi? (alama 3)

(e) Maneno na vifungu vifuatavyo vimetumika kwa maana gani kwa mujibu wa habari hii. (alama 3)

(i) Wakiziosha
(ii) Mbano
(iii) Mali
(iv) Kujifungua
(v) Maji hufuata mkondo
(vi) Kudondoka

**SEHEMU YA TATU: MATUMIZI YA LUGHA (Alama 50)**

3. (a) Bainisha matumizi ya -po- (alama 2)
(i) Achezapo hupendeza
(ii) Mtu hujikuna ajipatapo

(b) Kielezi kilichopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo kinaelezea juu ya nini? (alama 2)
(i) Msichana mrembo **kabisa** ameolewa
(ii) Wanariadha wale wanakimbia kasi **zaidi**

(c) Tunga sentensi mojamoja kwa kila kitenzi kifuatacho kuonyesha dhana amrishi. (alama 2)
(i) Tayarisha
(ii) Lala

(d) Andika katika usemi wa taarifa. (alama 2)
"Mtaondoka kesho asubuhi kwenda kwenu."
Mwalimu wetu alipofika hapa alisema.

(e) Ngeli ya u-zi inaweza kuainishwa kwa miundo mbalimbali ya nomino zake. Andika migawanyo yake minne huku ukitoa mifano miwili miwili ya nomino katika umoja na wingi.

(f) Zitaje ala mbili zitumiwazo kutamkia kila moja ya sauti hizi. (alama 2)

(i) /v/ ______________________________________________

(ii) /b/ ______________________________________________

(g) Sahihisha sentensi hii (alama 2)

Wewe haufai kuhairisha mkutano wa kuzungumzia madawa ya kulevya.

(h) Onyesha shamirisho ala, kitondo na kipozi katika sentensi ifuatayo. (alama 3)

Kijakazi alimpakulia chakula mwajiri kwa kijiko.

(i) Andika sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili tofauti ya ritifaa katika uakifishaji. (alama 2)

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

(j) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mtindo wa vielelezo tungo.

Mwanambuzi aliimba vizuri na mashabiki walishangilia sana.

4. (a) Tumia visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari kuandika sentensi ifuatayo upya. (alama 3)

**Ukuta** umemwangukia **mvulana** alipokuwa **akiuparaga**.

(b) Toa jibu sahihi kwa maamukizi yafuatayo. (alama 2)

(i) Sabalkheri ______________________________________________

(ii) Alamsiki ______________________________________________

(c) Vishimo vilivyochimbwa shambani ili kuweza kutiwa mbegu huitwaje? (alama 1)

(d) Chombo katika familia ya tarakilishi ambacho hubebwa na mtumizi wake na kuwekwa mapajani au mezani wakati wa kutumia kuwezesha kuchapisha, kupata habari za mtandao miongoni mwa huduma nyingine huitwaje? (alama 1)

(e) Ni nambari katika hesabu ambazo hugawanyika kwa mbili bila kubaki kama vile mbili, nne, sita na kadhalika. (alama1 )

(f) Kofia nyekundu yenye shada jeusi huitwaje? (alama 1)

(g) Mnyama kama kenge mwenye magamba mwilini ajikunjaye mithili ya mpira anaposhambuliwa huitwaje? (alama 1)

(h) Haya ni malipo gani? (alama 2)

(i) Maposa ____________________________________________________________

(ii) Kivusho ___________________________________________________________

(i) Chumba cha kulaza wagonjwa huitwaje? (alama 1)

(j) Mtu aliye na viungo vya siri vinavyodhihirisha jinsia zote mbili huitwaje? (alama 1)

(k) Tegua kitendawili hiki: (alama 1)
Hesabu haihesabiki

(l) Ni methali gani inayoeleza kuwa ni wajibu wa mwanafunzi kumheshimu na kumzawadia mwalimu ila si lazima kwa mwalimu kufanya hivyo. (alama 1)

(m) Fumbua fumbo hili (alama 1)
Jimbi alikuwa amesimama kwenye kichuguu
huku ameangalia mashariki. Je, yai alilotaga lilielekea wapi?

(n) Tunasema bunda la noti ilhali ______________________ ni kwa barua. (alama 1)

(o) Ni nini maana ya semi hizi: (alama 2)
(i) Kula mwande
(ii) Macho ya nje

**SEHEMU YA NNE: SAJILI YA LUGHA (Alama 10)**

5. (a) Kwa kurejelea Kiunguja, zitaje sifa zifaazo kwa lahaja kuteuliwa kama msingi wa usanifishaji wa lugha katika historia ya Kiswahili. (alama 5)

(b) Ni sajili gani ya lugha inayotokana na muktadha ufuatao. (alama 5)

(i) Mahakama ya juu ilishirikisha Mkuu wa Sheria kuhudhuria korti kama "amicurse Curie"

(ii) Ningependa mjitokeze kama mchwa na kumbikumbi siku hiyo. Tunaelewana? Kipepeo juu! Kipepeo juu!

(iii) Angalia ramani hiyo ya Afrika. Unaweza kunionyesha mto Kagera ulipo? Mstari wa istiwai unapitia nchi gani?

(iv) Nime --- wewe ---- fungua! Nikiingia uta ---- niona --- mimi si --- sichezi. Ba-ado unala --- lala. Fungua.

(v) Kumi! Kumi! Mali rahisi beba. Nguo kumi.

**M w is h o.**